Hemclock Sumu

Conium maculatum Familia ya Dania

Aina B Kwekwe Sumu: Inatakiwa kudhibiti kwenye Ardhi za Umma na Barabara

Namna za Kutambua

- Mmea mrefu wa kila miaka miwili (biennial), hufikia urefu wa futi 8 hadi 10 mwaka wa pili
- Majani kijani kibichi, yanafanana na kanganga (fern) na yana harufu kali, isiyovutia
- Mimea ya mwaka wa kwanza hukua katika vichaka vifupi; mashina ya madoa mekundu-zambarau
- Mashina ya mwaka wa pili yamevimba, yana mrija, hayana nywele, yana mbavu, na madoa au mistari mekundu-zambarau
- Mashina marefu ya mauwa yanafanya mashada (clusters) mengi yanafanana na mwavuli zenye mauwa mengi madogo
- Mbegu hutokea baada ya mauwa kwenye vidonge (capsules) vya rangi kijani na mistari ambavyo baadaye hubadilika rangi ya kahawa

Hemlock-sumu ina majani kijani kibichi na kanganga (fern) na yana harufu kali, isiyovutia.

Mashina mapana, bila nyewele yana madoa au mistari mekundu-zambarau.

Mafungu ya mauwa madogo meupe yenye petali tano hutokea mwisho msimu wa masika.

Biolojia

Hemlock-sumu huenea kwa mbegu. Mwaka wa kwanza hukua kiwaridi [rosette] (fungu la majani hariri karibu na ardhi). Mwaka wa pili humea mashina marefu na mauwa. Hukua upesi sana Machi hadi Mei na mauwa huota mwisho msimu wa masika (spring). Karibu mbegu 40,000 kwa kila mmea huota. Mbegu huanguka karibu na mmea na husambazwa na mmomonyoko, wanyama, mvua na shughuli za binadamu. Mbegu zinaweza kudumu kwenye ardhi kwa hadi miaka 6 na huota msimu wote wa kupanda.

Matokeo

Sumu sana kwa watu, mifugo, na wanyama pori,; inasababisha kifo kwa kupooza kupumua baada ya kula. Zinakuwa kwa nguvu sana hata inakandamiza mimea mingine mizuri inayohitajika. Huanza kumea mapema na ni rahisi zaidi kuliwa na wanyama kukiwa na uchache wa majani na nyasi. Mimea inaweza kufananishwa na karoti, haswa ikiwa midogo.

Kuenea

Aina ya Eurasia, inapatikana kwote Amerika Kaskazini. Mimea imesambaa kwote King County; iko ukingo wa barabara, sehemu za mito, mabonde, viwanja, mashimo na viwanja bila majengo. Hupendelea udongo mbichi, lakini inaweza kuzowea udongo mkavu na kivuli.

Unachoweza Kufanya

Ondoa hemlock ya sumu na fahamisha yeyote anayetumia sehemu hiyo, haswa sehemu zinazopita watu, wanyama wa nyumbani na mifugo. **Sehemu zote za mmea ni sumu zinapoliwa na hata shina zilizokufa huendelea kuwa sumu kwa hadi miaka mitatu.** Kila mara vaa nguo za kujikinga (glovu, mikono mirefu) unapoondoa mmea huu. **Ukishuku sumu, omba usaidizi haraka sana.** Kwa binadamu na wanyama, matibabu upesi yanaweza kurudisha nyuma madhara ya sumu ya hemlock. Unaweza kuripoti maeneo kwenye ardhi za umma na barabara kwa Programu ya King County ya Kudhibiti Kwekwe Sumu (King County Noxious Weed Control Program).

Namna ya Kudhibiti

Kutumia Mikono:

Vaa glovu na nguo zenye mikono mirefu. Kwa sehemu ndogo, ng'oa au chimba mimea. Toa mzizi wote. Nawa mikono yako vizuri baada ya kugusa mimea. Ili kufaulu, mimea yote iliyokomaa inahitaji kutolewa ili kuzuia mbegu mpya. Ukishasafisha eneo, mwaga tandazo (mulch) au panda mimea mingine inayostahili. Itasaidia kuzuia mbegu za hemlock sumu zisichomoze tena. Usiwache vichwa vya mauwa kwenye mchanga kwa kuwa mbegu zinaweza kuzaa mimea mipya. Kutengeza mbolea sio jambo zuri; badala yake weka mimea iliyong'olewa kwenye mifuko ya takataka na utupe kwenye taka zako za kawaida.

Kutumia Mashini:

Tahadhari: sumu zinaweza kuingia kwa pua wakati hemlock sumu inapokatwa kwa mashini. Kukata kwa mashini au kwa panga sio vyema kwa hatari ya kupumua sumu. Pia, mimea iliyokatwa na mashini inaweza kumea tena kwenye mizizi.

Dawa za Kemikali:

Fuata maagizo ya kibandiko (label) kikamilifu na utumie tu bidhaa zinazostahili tena halali kwa eneo hilo. Dawa ya kuuwa kwekwe itumiwe tu kwa kiasi kilichoagizwa kwenye kibandiko. Nyunyizia mimea (majani na mashina) msimu wa masika, na ufuatilie tena baadaye msimu wa kiangazi kwa mimea ya msimu. Nyunyizia mimea kabla mauwa kumea ili upate matokeo mazuri zaidi. Kunyunyizia huenda kusizuie mimea iliyokomaa isitoe mbegu. Kwa sehemu zenye nyasi tunapendekeza kutumia dawa ya kuuwa kwekwe inayochagua (selective) ya majani mapana ya dawa ya triclopyr, 2,4-D au metsulfuron. Bidhaa za glyphosate pia zitafanya kazi lakini zitauwa nyasi pamoja na mimea ya majani mapana. Usikate mimea iliyotiwa dawa hadi itakapokufa. Mbegu huota msimu mzima, kwa hiyo ni muhimu kurudia dawa ili kuangamiza mimea yote. Namna za kudhibiti na kemikali huenda zikawa tofauti kwa matumizi binafsi, ya biashara na serikali. Kwa maelezo zaidi, wasiliana na Programu ya Kudhibiti Kwekwe Sumu (Noxious Weed Control Program).

***Mimea midogo hufanana na karoti, lakini sehemu zote (mizizi, mashina, mauwa, mbegu, majani) ni sumu.** Vaa nguo za kulinda na ufanye makini.*

Huenea upesi sehemu wazi, huondoa mimea ya manufaa.

Inaweza kufananishwa na:

Karoti Mwitu (*Daucus carota*) na mimea mingine ya familia ya dania, pamoja na shamari (fennel), chervil na anise hufanana na Hemlock Sumu.

Karoti mwitu inaweza kutofautishwa na hemlock sumu kwa njia kadhaa. Karoti mwitu kawaida humea tu urefu wa futi 3; mashina yake ya kijani cha kawaida yana nywele nyepesi na matawi machache; na huota muawa baadaye msimu wa kiangazi. Lakini, hemlock sumu hukuwa kufikia urefu wa futi 8 au zaidi; majani yake hutoa harufu kali isiyopendeza; na mashina yake bila nywele yana madoa/mistari mekundu au zambarau.

Karoti mwitu (yaani Queen Anne's Lace) kawaida hufananishwa na hemlock sumu.

Mapema msimu wa masika, tafuta matuta ya majani hariri ya rangi ya kijani cha kung'ara. Mafundo makubwa zaidi ni ya mimea ya mwaka wa pili inayovuta kasi kumea mauwa na kutoa mbegu baadaye msimu wa masika.

Picha ya karoti mwitu ya Andreas Rockstein / CC BY 2.0.
Faili: NoxWfact-Poison-Hemlock-2018.indd

206-477-WEED (206-477-9333) or TTY: 711
kingcounty.gov/weeds **noxious.weeds@kingcounty.gov**

King County